# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA SABA

**07 FEBRUARI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 07 FEBRUARI, 2024

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**107. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali imefanya tathmini ya mafunzo wanayopatiwa Vijana chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya kumaliza mafunzo hayo.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**108. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya kupeleka Majokofu manne ya Mochwari kwenye Kituo cha Afya Mugeta.

**109. MHESHIMIWA NORA WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itamalizia ujenzi wa Zahanati ya Uwanja wa Ndege katika Kata ya Mafisa Mkoani Morogoro.

**110. MHESHIMIWA HAMISI SHABANI TALETALE (MOROGORO KUSINI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ngerengere.

## OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

**111. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuvutia Wawekezaji kujenga Viwanda vya Maziwa Mkoa wa Arusha.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**112. MHESHIMIWA STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka alama za kuongoza meli katika eneo la kuegesha meli kwenye Ziwa Nyasa.

**WIZARA YA KILIMO:**

**113. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaweka utaratibu wa mbolea kuwekwa kwenye vifungashio vya kilo 5, 10, 15, 25 na 50.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**114. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Tanzania itajiunga na Mkataba wa *Budapest* ili kujiimarisha na mapambano dhidi ya makosa ya kimtandao.

**WIZARA YA UJENZI:**

**115. MHESHIMIWA SHANIF MANSOOR JAMAL (KWIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza mchakato wa kutangaza Barabara ya Mabuki-Jojiro hadi Ngudu ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

**116. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini miundombinu ya mipaka ya nchi yetu itaboreshwa ili kukuza Diplomasia ya Uchumi na nchi zenye fursa za kibiashara kama DR – Congo.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**117. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, mchakato wa kuwa na Vazi la Taifa umefikia hatua gani.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**118. MHESHIMIWA MOHAMED JUMAH SOUD (DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, utaratibu gani unaotumika kwa Kamandi mbalimbali nchini kuanzisha miradi ya kibiashara katika maeneo ya Kamandi.

## WIZARA YA MADINI:

**119. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ipo tayari kufanya utafiti wa Madini katika Kata ya KIA Jimbo la Hai.

## WIZARA YA MAJI:

**120. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itaanza kuunganisha mita za maji za kulipia kabla ya matumizi kama za TANESCO Arusha Mjini.

**121. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa maji wa Tukuyu utakamilika.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**122. MHESHIMIWA REUBEN NHAMANILO KWAGILWA (HANDENI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itapeleka Gari la Zimamoto Handeni Mjini.

**123. MHESHIMIWA ABDI HIJA MKASHA (MICHEWENI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Kituo cha Polisi Micheweni kitakarabatiwa ili kiendane na hadhi ya Wilaya.

**WIZARA YA AFYA:**

**124. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusamehe gharama za matibabu kwa Marehemu ili kupunguza maumivu kwa Wafiwa.

**WIZARA YA NISHATI:**

**125. MHESHIMIWA NDAISABA GEORGE RUHORO (NGARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka umeme kwa Wananchi wanaoishi kwenye mitaa 17 ya Mamlaka ya Mji Mdogo Rulenge - Ngara.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**126. MHESHIMIWA YAHAYA OMARY MASSARE (MANYONI MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, ni Malambo/Mabwawa mangapi yatajengwa katika Halmashauri ya Itigi kwa ajili ya kunyweshea Mifugo.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2023.

**DODOMA** **N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**07 FEBRUARI, 2024** **KATIBU WA BUNGE**